SHUGHULI ZA KISWAHILI - GRADE 4 EXAMS TERM 2 2023

MAAGIZO

- Karatasi hii ina sehemu tano kuu.
- Jibu maswali yote kulingana na maagizo.

MASWALI

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.
Fanaka ni mwanafunzi katika shule ya msingi ya Elimubora. Yeye hupenda sana kuvaa nguo safi. Rinda lake huwa nadhifu na kupigwa pasi hadi likapendeza. Fanaka anajulikana katika shule yote kutokana na tabia zake nzuri. Anapokuwa shuleni, yeye huwa na marafiki wa karibu wawili. Marafiki hao ni Mwanzia na Kalondu. Yeye na marafiki zake husoma pamoja, kucheza na kula pamoja. Wao hupenda sana kucheza kibemasa. Wanapokuwa darasani, hawawezi kuenda haja bila kuomba idhini. Wanapotoka haja, wao huhakikisha kuwa wamenawa mikono kwa maji safi na sabuni.
Kule nyumbani, Fanaka hupenda sana kucheza na mnyama ampendaye ambaye ni paka. Paka wake ana rangi nyeusi na nyeupe. Fanaka humpa paka wake maziwa na nyama. Anapokuwa mgonjwa, paka huyo hupelekwa kwa daktari wa mifugo ili ampime na kumpa. matibabu Fanaka pia huwasaidia wazazi wake kufanya kazi za shambani na za nyumbani. Ndugu zake wawili hawajaanza kuenda shuleni kwa kuwa bado hawajafikisha umri wa kujiunga na shule.

1. Fanaka na wenzake hunawa mikono kwa maji
    A. safi.
    B. moto.
    C. mengi.
    D. baridi.
2. Ni kweli kuwa Fanaka ni
    A. mfupi.
    B. mvulana.
    C. msichana.
    D. mrefu.
3. Nahau 'kuomba idhini' ina maana gani kulingana na ufahamu?
    A. enda msalani
    B. omba ruhusa
    C. toka nje
    D. chukua nafasi
4. Fanaka na wenzake hunawa mikono;